**Jiwe la kiroho la kujengea na 27**

# LI NENO NI ROHO ROHO KATIKA NAMNA YA NENO

***Enenda katika Roho.***
***Yohana 6:63………. " Maneno hayo niliyowambia Roho tena uzima"***

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema kuhusu hilo: Kama vile divaini ya asili inavoojiioonesha yenyewe katika nguvu ya msisimko, Kadhalika ndivyo inafanyavyo divai mpya inapolifunua neno la Mungu ambalo ni Roho
***(Ufunuo 6:6)*** Hilo maana? Neno lenyewe ni Roho. Unaamini hilo? Hebu tusome hilo, Roho ndo itiayo uzima mwili haufai kitu, maneno hayo niliyowaambia ni Roho tena ni uzima***" (Yohanna 6:63) .***

Lile neno lenyewe ni Roho katika umbo la neno na sasa unaona waliali linapohusishwa au linapotiwa uhai ile Roho ya neno inaingia kazini na kutenda unaona? Sasa angalia hapa: wazo inabidi liwe wazo kabla halijawa neno. Na sasa wazo linapowasilishwa linakuwa neno. Sasa hili ni wazo la Mungu ambalo ameliweka katika neno na sasa tunapolipokea hilo hutokea kwake, linakua neno.

Mungu alimfunulia Mussa kipaswacho kufanya, Mussa akalinena hilo, na likatokea ***(Kutoka 14:13-31)*** Unaona? Hilo ndilo hasa linapotoka hasa kwa Mungu….Sasa, tunaona inaleta msisimko, na inaleta furaha, ni kwa sababu ni neno la Mungu, na ile divai mpya inasisimua. ***(Luka 5:36) …*** Inapofunua neno halafu inaleta furaha isyopimika wakati mwingine inaleta furaha mpaka inafurika . [1]

Alizungumzia wakati huu, kile ambacho kingekuweko sasa. Waaminio wa wakati huu, inabidi waamini hiki kilichoahidiwa katika siku ya leo kama vile ambavyo walipaswa waje kwenye safina ili waokolewe, watoke Misri ili waokolewe, inawapasa waje ndani ya Kristo ili waokolewe sasa. Ndani ya neno, ujumbe. Kwamba Yeye ni yule jana na hata milele [2]

Mungu hata iokoa dunia kwakutumia madhehebu/ utaratibu fulani. Ataiokoa dunia kwa Roho Mtakatifu na Roho Mtakatifu ni neno linapoodhihirishwa ni ahadi za Mungu zinapodhihirishwa. [3]

Tunda la Roho ni neno la Mungu linapojidhihirisha lenyewe, upendo, furaha,amani,uvumilivu,utu wema,subira,imani.Imani katika nini? katika neno ***(Wagalatia 5:22-23)*** [4]
Roho Mtakatifu leo anatawala na Roho Mtakatifu ni neno [5].

Sasa adui anaposhambulia na kujaribu kusema unapaswa kusema hivi ufanye hivi na ufanye vile, utaenda kufanya nini? Kaa simama na neno hio ni sawa unataka ufanye nini hapo tena? Lichukuwe neno. Neno ni nini? Bibilia ilisema hapa kwamba Roho wa Mungu ni neno unaona,angalia hapa " Chukuwa chepeo ya uokovu na upanga, Upanga wa Roho" Ni Roho gani inayokuja kupitia nia yako na kuingia ndani yako na upanga wa hivyo Roho ni neno la Mungu ***(Waefeso 6:17)*** Roho anapigana kwa kutumia nini, Roho Mtakatifu anapigana kwa kutumia nini? Msisimko?Kujisikia?Neno.Utukufu. Anapigana kwa Kutumia nini? Neno la uponyaji neno.Hebu tuseme neno. Neno la Mungu ndilo ambalo analitumia kupigana. Roho wa Mungu anatembea moja kwa moja kwa Shetani na Kumwambia imeandikwa" Ameni. " Ameandikwa" kuwa na Shetani anaondoka ***(Mathayo 4:1-11)*** [6]

Yesu kamwe hakumsikiliza yeye. Na kama hakumsikiliza wakati huo,hata watu wake pia hawatamsikiliza yeye. Muache apige kelele,hatujali.Tunatembea katika Roho wa Bwana [ 7]
Kwa sababu Yesu alisema "Kama tukiongeza neno moja kwa hili au tukiondoa neno katika hili sehemu yetu itaondolewa katika ule mti wa uzima"
***(Ufunuo 22:18-19).*** Unaona siyo hata neno moja inatupasa tulichukue hivyo hivyo kama lilivyo andikwa na Mungu analiangalia neno lake ili kulitimiza hilo.
***( Jeremia 1:12).***

Natunajua kwamba linapaswa liwe sahihi kwa hiyo haijalishi kanisa lolote, linasemaje, haijalishi mtu mwingine yeyote anasemaje kama wewe umezaliwa na Roho wa Mungu ***(Yohana 3:3-8)*** unakuwa sehemu ya Bibilia. Mungu alimwambia Ezekiel Nabii "chukuwa hilo gomba na ulile" halafu nabii akawa ni kitu kimoja na lile gomba***" (Ezekiel 3:1-4)*** na huyo ni mwaminio anapopokea Roho Mtakatifu aliandika Biblia na Roho wa Mungu ni neno la Mungu "Maneno yangu ni Roho, hapo mwanzo kulikuwepo neno naye neno alikuako kwa Mungu naye neno alikuwa ni Mungu naye neno akafanyika mwili akakaa kwetu. ***(Yohana 1;1-2:14)***
***(Waebrania 13: 18)*** "Yeye ni yeye Yule jana leo na hata milele" Na unapokuwa sehemu ya lile neno ooh! Wanacho kitu Fulani kije kinyume na hilo neno kuna kengele ndogo inalia haraka sana unaona? Ni onyo la kukuambia kwamba kifo kiko njiani kwamwe hatupaswi kufanya hivyo [8]

Sasa Roho Mtakatifu ni neno, Mungu sio watatu, ni Mungu Yule Yule katika nyakati zote tatu, Ofisi tatu. Mungu, Yule baba juu ya sheria, Mungu, Yule mwana, katika wakati wa neema, Mungu, Roho Mtakatifu, kama mnavyoliita hilo Mungu Yule Yule, wakati wa Roho Mtakatifu.
Mungu, Baba,Alikuwa ni neno,Mungu, Mwana, Alikuwa neno, Mungu, Roho Mtakatifu alikuwa ni neno. Unaonaje? ni zile ofisi tatu tu ***(1Timotheo 3:16)(Waefeso 4:4-6)***na Roho Mtakatifu anapokutia muhuri, umetiwa muhuri na neno. ***(Waefeso 1:13-14)*** [9]

Unasema “vema, watu wengine wanafanya hivyo” wewe siyo kama watu wengine. Wewe umekufa na uhai wako umefichwa ndani ya Mungu kupitia Kristo, na ukitiwa muhuri na Roho Mtakatifu ***(Wakorosa 3:1-2)*** Unaona? Huku jarbu ila sumu. Ni kwasababu watu hawataki kujaribu hilo. Sasa inakupasa kufa, inakupasa kuoza.***(Yohana 12:24-25)*** Hiyo ndiyo shida ya watu baada yake wanaenda madhabahuni na kupata msisimko Fulani, wanaruka na kutingisha mikono yao na kupeana mikono na mhubiri halafu wanatoka na kwenda kuchukua fundisho la kanuni, Ungano na kuanza kulikalili hilo na kusema “Mimi ni wafulani na fulani” wewe ni mkristo? Mkristo anapaswa kuwa kama kristo kuwa kama Kristo ni kuamini neno, kama huliamini hili neno huwezi kuwa kama anayefanana na Kristo. Utawezaje kusema wewe ni Mkristo na ukatae nusu ya neno? Kama Roho Mtakatifu aliandika neno, Roho Mtakatifu analithibitisha neon, na Roho Mtakatifu neno na neno likikaa ndani yako. Inazileta ahadi za Mungu kwa kila mwaminiyo ***(Yohana 15:7)*** Amina! hilo neno linamaanisha na iwe hivyo inaliamini hilo kwa moyo wangu wote. Ni neno la Mungu aliyehai. Ameen! [10]

“Ulisema neno ni Roho?” ndiyo, bwana. Mungu alisema neno langu ni Roho, Hiyo ni sawa. Bibi Harusi wakweli ni sawa lazima aunganishwe na neno.sasa kumbuka kama Yeye ni sehemu ya Kristo lazima awe ni neno Kristo. Ili awe neno Kristo inabidi ubatizwe ndani ya Kristo ***(1 Wakorintho 12:13)*** Na unapokuwa ndani ya Kristo, unamuamini Kristo na Kristo ni neno [11].

Na pale utakuja wakati ambapo atajieleza mwenyewe katika ukamilifu kichwa wa Ungu.Kupitia kanisa lake. Awe na nafasi ya kwanza katika kanisa lake.
***(Wakoosai 1:16-19)*** ooh! Jamani ni nini? Yule mtu aliyepakwa mafuta.Sasa ni watu waliopakwa mafuta. Wamepakwa mafuta kwa kukubali kile ambacho hawa na Adam walikishindwa , wanarudia upako wa lile neno kwa sababu alisema neno langu Roho unaona , kile Hawa alishindwa. Yeye anakuja na Fisi tunakubali. [12]
Warumi 8:1 “Sasa basi hakuna ya adhabu juu ya wale walio” wale wanaliamini hilo ni wale walio ndani ya Kristo Yesu “Ambao hawaenendi kwa kuufuata mwili bali Roho wale ambao hawasikilizi dunia inachosema na maneno yangu ni Roho na uzima. Hata kama unaumwa Daktari amesema “Unaenda kufa” husikilizi hilo halikusumbui hata kidogo. Kama wanakuambia “Inabidi uwe mkatoliki kabla ya kuokolewa au uwe Mpresbitaria kabla ya kuokolewa” Hulisikilizi hilo “kwahiyo hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu ambao hawaufuati mwili. Mambo yale unayo yaona” mambo yote unayoyaona na macho ni mambo ya dunia lakini ni yale mambo unayoyaona katika Roho yako, Kupitia neno? Lile neno ni kioo cha Mungu cha kuangalia na kuakisi kile alicho na kile ulicho, Haleluya oh! Jamani ninakwambia wewe, Hiki ni kitabu cha pekee duniani kinachokuambia umetoka wapi, wewe ni nani? Na unaenda wapi. Nionyeshe ukursa wowowte wa maandiko popote pale, pamoja na sayansi yote au kitu kingine chochote,kitabu kizuri chochote kilichowahi kuandikwa hakuna na hata

kimojawapo kinachoweza kukuambia hilo. Hiki ni kioo cha mungu cha kuangalia kinachoonyesha alicho na kile ulicho(13)

Tunabatizwa ndani ya hekalu la Mungu ***(1 Wakorinto 6:19-20)***ndani ya mwili wa Mungu wa Yesu kristo na tunakuwa ndani ya kristo kwa ubatizo wa Roho mtakatifu ***(1 Wakorinto12)***“Na kwahiyo hakuna hukumu ya adhabu kwa hao walio ndani ya kristo Yesu ambao hawaendi kwa kufuata mwili bali Roho”
***(Warumi 8:1)*** wanatamani mambo ya kristo hawajali mambo ya mwili. “Mwili wangu unasema nimechoka sana”, “Roho yangu inasema wewe hujachoka , mimi ndio bosi wako unifuate mimi” unamatatizo pale na dactari anasema kwa tatizo hili hawezi kupona, hiyo kesi imeisha”nitamuangalia yeye na kusema hiyo nisawa. Lakini Roho mtakatifu anakuja na kunipa maono na kusema “Anaenda kupona”Hapo ninasema “Hii aseme bwana huyu mtu ataishi”Nasi hatutembei kwa kufuata mabo ya mwili tena kila mabo mwiliunasema (Kama vile kupigana vita na machafuko, kila kitu, mambo ya kibnafsi) au kile ambacho macho yanaonana na kile ambacho masikio yao yanasikia, tunatembea kwa kufuata mabo ya Roho hiyo ni sawa(14)

Sasa mwili wetu imetengenezwa kwa madini aina kama sita za duniani tunajua hiyo imetengenezwa kwa portasium na kalsium na prolium na nuru ya kosmik na chembe chembe za atom na kudhalika zote zimekusanywa pamoja na kuufanya huu mwili zinazotoka kwenye mavumbi ya dunia unakula chakula na kadri unanyo zidi kula chakula kinageuka kuwa mavumbi na kinatokana na mavumbi na huo mzunguko huendelea oh kijana unautukuza mwili lakini ile Roho inanafsi iliyoko pale nyama yangu ni kama ya mnyama tu na kama unatamani mwili na mambo yanayo yaona kuwatamani wanawake kutamani vitu hivi tofauti bado na mnyama hiyo ni sawa hupaswa kufanya hivyo Roho wa mungu atakuongoza mbele na kukuweka mahali pa juu zaidi ya hapo ***(Wagalatia 5:16-21)***hiyo ni sahihi kabisa (15)

Hawajali dunia insemaje au mtu mwingine anasema nini au hata familia zao zinasema nini wanatembea katika Roho wa mungu katika upendo mkamilifu wa mungu unaona?(16)

“Wanaoongozwa na roho wa mungu ndiyo wanawa Mungu” ***(Warumi 8:14)***sasa hii sehemu ya kibinadamu inapoondoka na Roho wa Mungu unajaza hiyo nafsi, mahali ambapo unajimwaga mwenyewe au mahali ambapo unajifanya si chochote (Amina) Hapo ndipo kanisa litakuwa kutakuwa katika nguvu za kufufuka kwa Bwana Yesu, watatembe katika hatua zake, katika nguvu zake, katika mawazo yake, katika utu wake katika utendaji wake……………………unaona ninichomaanisha ? hapo sasa mawazo yako yatakua ni maneno na maneno yatakuwa vitu vinavyoonekana hapo ndipo kanisa litakuwa katika nguvu

zake……………..ni namaanisha liko njiani, hapo ndipo kanisa litakapo kualimefungwa ndani ya kristo, Roho mtakatifu mwanadamu atakuwa mbali na wao wenyewe, kwamba hawajioni wenyewe hawana mawazo ila kumtumikia Mungu na mawazo yao yataendelea wakatoa mambo ya ulimwengu watatembea katika Roho watapiga hatua katika Roho hivyo kutimiza sheria ya kristo (wagalatia 5:16) Hapo sasa upendo wa Mungu uko ndani ya moyo wa mwanadamu wakitembea katika Roho ***( Warumi 5:5)***Hilo kanisa kuu la ajabu litaenda mbele na nguvu na uungu kwa sababu uungu utafunguliwa kwa wanadamu kwa Roho mtakatifu ikiyafanya mawazo yao yaliyoko ndani mwao yatimie. (17)

“Angalia kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa na kuwa washindi wa mwili huu” na mtu aliyoko ndani ya kristo Yesu anatembea akifuata mambo ya kiroho kwa wa dunia na kitu cha mwili ni upuuzi lakini kwa wale wanaoamini ni uzima wa milele (Amen) tuko hapo oh ni zuri kiasi gani kitakuhukum wewe uko na Kristo Yesu ***(Warumi 8:37-39*****)** Kama ilivyo hakika kwamba Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu, tutakuja ndani ya Yesu Kristo, (Amina) ndiyo ni lazima iwe hivyo Mungu tayari ameahidi hilo.Kama ilivyo hakika kwamba ule mwili utakwenda juu, na mimi niko ndani ya ule mwili nitaenda pamoja nao . [18]

Na ukifanya kitu chochote ambacho ni makosa siyo kwa kukusudia (1 waraka Yohana 3:9) hutendi dhambi kwa makusudi mtu anayatenda dhambi kwa makusudi anatoka nje na anatenda dhambi kwa makusudi kamwe hajaingia kwenye ule mwili bado***(Waebrania 10:2)***lakini mtu akiingia pale amekufa na maisha yake yamefichwa ndani ya Mungu kwa njia ya Kristo yametiwa mhuri na Roho Mtakatifu (Wakolosai 3:1-3) na Shetani hawezi kumpata Yeye yuko mbali sana nyuma kule inabidi atoke nje kule alipo kabla ya shetani hajaweza kumpata Yeye kwa maana umekufa. [19]

“Yeye aliyezaliwa na Mungu hawezi kutenda dhambi” ***(1 Waraka wa Yohana 5:18)Warumi 8:1,***“Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu wasio nenda katika mwili bali katika Roho: Tuko hapa unaona hiyo unafanya mwili wako unatishiwa huhitaji kusema “oh! Kama ningeacha tu kulewa! kama ningeacha ………..” ingia tu ndani ya Kristo na hivyo vyote vitaondoka unaona, kwa sababu mwili wako unatiishiwa na Roho haufati tena mambo ya dunia umekufa. Wamekufa; dhambi zako zimezikwa katika ubatizo ***(Warumi 6:3-4)***na wewe ni uumbaji mpya ndani ya Kristo ***(2 Wakorintho 5:17)*** na mwili wako unatishiwa na Roho ukijaribu kuishi maisha yaliyo sahihi. [20].

Oh ndugu hili neno ni uhai kama utalishikilia angalia siyo kitu tu tunakizungumzia ambacho kitatutokea hapa na pale ni kitu ambacho tayari kiko na sisi na kinatokea sasa siyo kitu Fulani kitakuwa ni kitu ambacho kimekwisha kuwa hatujaribu kishahuhudia “ tunajua kile alicho kifanya ; tunajua kile anachoenda kufanya” Lakini sasa tunaeleza kile ambacho anakifanya unaona? Hii ni saa yetu. Tunaweza tusiishi kuuma unyakuo ninaweza nikafa leo unaweza ukafa leo mimi

sijui lakini unyakuo unakuja hapo ndipo hilo linakuja, tutakua pale, usiwe na wasiwasi kadhalika wale wengine wote kule nyuma katika nyakati zote, ambao wameamini na kutazimia hilo ***(1 –Wathesalonike 4 :13-17)*** walitembea katika nani ya wakati wao. Na hapa sasa ipo nini Yesu Kristo Yule jana leo na hata milele acha kanuni zako na amini hili neno hii ni kweli neno ni kweli ***(Yohana 17:17)*** Yesu alisema " Neno langu ni Roho na neno langu ni uzima? Unaendaje kupokea ungamo ambalo ni mauti na neno la uzima? Utawezaje kupokea vitu viwili wakati huo huo huwezi kufanya hivyo "Ebu kila neno la mtu liwe uongo na kila ungamo liwe uongo" Neno la Mungu ndiyo kweli. [21]

Kama moyo yetu haitahukumu ***(1 Waraka wa Yohana 3 :20-22)*** tuko hapo toka hapo lakini kaa na lile neno ambacho ndani ya hilo hakuna kinacho hukumiwa hakuna hukumu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu ambao hawaendi kwa kufuata mwili lakini kwa Roho anaongoza kwa neno kwa sababu Roho inaweza ikaja tu kupitia kwenye neno kwa sababu Roho inaweza ikaja tu kupitia kwenye neno kwa sababu neno ni Roho wa kweli wa Mungu anaweza akazungumzia tu neno la kweli la Mungu. [22].

Lakini Paulo alisema kama nitaimba katika Roho kama nitahubiri nitahubiri katika Roho kama nitatembea nitatembea katika roho kama nitazungumzia nitazungumza katika Roho. " Hebu kila kitu kifanyike kuwa neno na kwa Roho ndiyo Bwana (Amina!) Hiyo yote ni kweli ya Mungu. [23]

Kusudi lako lote ni Kristo unamuangalia yeye kuja dakika yoyote unatembea katiak Roho: unampenda yeye unamuona yeye akitenda kupitia wewe siyo chochote unchotamani kufanya lakini analifanya hilo mwenyewe oh! Ni wakati gani [24]

Kitu kikuu mno nilichowahi kuona katika maisha yangu ni kujisalimisha wewe mwenyewe kwa Mungu na kutembea katika Roho siku baada ya siku kile atakavyo kuongoza wewe na kufanya mambo sasa basi hakuna hukumu kwa hao waliondani ya Kristo Yesu, kwa kuwa hawaendi kwa kufuata tama za mwili wanaenda kwa Roho na kama unampenda bwana unapenda kufanya kila kitu unacho wezi kufanya kila kitu unachoweza kufanya kumpendeza yeye [25]

Kama Izraeli kule nyuma katika nchi yao ya ahadi hajui amefikaje pale amewekwa tu automatiki pale nyuma kuaminio nguvu ya kitaifa ili muweka yeye mahali pale sasa ninaenda kusema kitu Fulani nguvu ya taifa ilimuweka Izaraeli katika nchi yake ya ahadi nguvu ya kitaifa iliweka kanisa katika baraza la makanisa duniani: lakini nguvu ya Mungu itawaweka watu katika bibi anisi nguvu ya dunia dunia insukuma upande huu na dunia inasukuma upande huu lakini Mungu anasukuma kwenda juu, Roho wa Mungu ambae na neno la Mungu neno langu ni Roho na uzima litamuweka bibi arusi mahali pake kwa sababu atatambua nafasi yake katika neno hapo atakua yako ndani ya Kristo litamuweka

yeye mhali pake hakuna nguvu za kitaifa zitakazo fanya hivyo lakini nguvu za kitaifa ziliwapeleka Izraeli katika nchi yao ya ahadi nguvu za kitaifa za baraza la makanisa zitaendesha kila dhehebu lingine ndani yake lakini nguvu za Mungu zitamuinua bibi birusi kwenda utukufuni kutoka katika hilo oh! Watu, tambueni siku yenu kama Yesu alivyowaonya: ile ishara ya Sodoma na hali ya makanisa ya siku ya leo [26]

Hebu tuingie ndani ya Kristo neno kwa maana tumelitaka hilo kwa jina lake na kwa utukufu wake (Amina)

<u>**Nukuu za kimaandiko**</u>

1) Mhuri wa nne (63-0321) uk. 288
2) Makali alipochagua Mungu pakuabudia (65-0220) aya, 91
3) Dunia inamomonyoka vipande (63-0412m) aya 88
4) Presuming (62-0610m) aya E-202
5) Kwanini Bethlehemu mdogo (63-1214) aya 161
6) Vita vikuu vilivyowahi kupiganwa (62-0311), uk 57
7) Kipofu Bathmayo (59- 1127) aya E-27
8) Kiu ( 65-0919) aya 63-64
9) Nitafanya nini na Yesu aitwaye Kristo ? (631124m) aya 104
10) Kwanini? (62-0622E) aya E-41
11) Ugomvi kati ya Mungu na shetani (62-0531) aya E-73
12) Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa (63-0728), aya 380
13) Waebrania sura 5-6 ( 57-0908) aya (109-112) aya 109-112
14) Kitabu cha mwanakondoo cha uzima (56-0603) aya E-50
15) Waebrania sura 1 (57-0821) aya 162-163
16) Kitabu cha mwanakondoo cha uzima (56-0603) aya E050
17) Neno limefanyika mwili 954-1003m) aya 183
18) Israeli na kanisa 2 (53-0326) aya 30
19) Kufanywa wana 4 (60-0522E) aya 54
20) Huyu melekizedeki ni nani (65-0221E0 aya 71
21) Lile shtaka (63-0707m) aya 260-262
22) Uzao wako utimilifu milango ya adui zao 962-021m) aya E-78
23) Kufunuliwa kwa Mungu (64-0614M) aya 378
24) Kusikia kutambua na kulitenda kazi neno la Mungu (60-0221) aya 230
25) Tangu wakati ule (60-0716) aya E-26
26) Kutambua siku yako na ujumbe wake (64-0726M) aya 192-193
27) Kwanini ilikuwa wachungaji 964-12210 aya 1

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 27 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju.*
*Box 553 Korogwe -  Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*